035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA
# LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
- A. waraka
- B. barua maalum
- C. barua ya kiofisi
- D. Barua rasmi

Jibu sahihi ni **D**

**Katika karatasi ya majibu:**

**2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Zawadi alikuwa msena wangu wa dhati ___1___ kwa mengi. Hakika huyu ni ___2___ watu muhimu ___3___ kukutana ___4___ maishani mwangu. Alipoona nikikaribia kukata tamaa, alinihimiza niwe ___5___. Akanikumbusha kuwa ___6___; kulishinda jambo ___7___ humhitaji mtu kutia bidii na kujaribu tena na tena. Kwa njia hiyo, ___8___ masomoni hasa katika Kiswahili. Niliweza kuvitambua vihusishi kama vile, ___9___.

1. A. alionifaa B. alivyonifaa C. aliyenifaa D. aliponifaa
2. A. kati ya B. baadhi ya C. miongoni ya D. dhidi ya
3. A. niliyewahi B. niliowahi C. aliowahi D. ningewahi
4. A. naye B. nawe C. nami D. nao
5. A. mwadilifu B. mkakamavu C. mtiifu D. mwangalifu
6. A. Mchuma janga hula na wa kwao B. Mkono mmoja haulei mwana C. Papo kwa papo kamba hukata jiwe D. Kijaacho tele hutawanyika
7. A. ngumu B. kali C. nzito D. gumu
8. A. niliimarika B. niliimarisha C. niliimarishwa D. niliimarikia
9. A. sana, tele, aghalabu B. ingawa, japo, almradi C. kando ya, tangu, katika D. yule, hiki, hivyo

Bara la Afrika lina ___10___ mataifa ___11___. Japo mengi ya haya yamebarikiwa kwa maliasili kama vile ___12___, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba ___13___ wa bara hili wangali ___14___ katika lindi la ufukara. ___15___ takwimu zinazotolewa mara kwa mara, umaskini huu unachangiwa pakubwa na uongozi duni.

10. A. takriban B. yamkini C. nusura D. hadi
11. A. hamsini na nne B. hamsini na tano C. hamsini na tatu D. hamsini na matano
12. A. dhahabu, mafuta na miundomsingi B. mito, mabonde na madini C. utandawazi, mbuga na nyika D. wanyamapori, umeme na milangilangi
13. A. raia B. walowezi C. wakazi D. wazalendo
14. A. wanajitosa B. wanasisitiza C. wanafarakana D. wanaselelea
15. A. Kwa mujibu wa B. Zipo C. Kama D. Angalau

*Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

16. **Ainisha maneno yaliyoangaziwa katika sentensi hii.**
Mvulana huyo **hodari** alipanga kazi yake **vizuri**.
A. kiwakilishi, kielezi
B. kivumishi, kielezi
C. kivumishi, kiwakilishi
D. kiwakilishi, kihusishi.

17. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
Jiko hilo liliangukiwa na ua ulipobomoka.
A. Majiko hayo yaliangukiwa na maua yalipobomoka.
B. Meko hayo yaliangukiwa na ua ulipobomoka.
C. Majiko hayo yaliangukiwa na nyua zilipobomoka.
D. Jiko hizo ziliangukiwa na maua zilipobomoka.

18. Malipo au zawadi inayotolewa katika sherehe ya kumshika mtoto mchanga huitwa
A. arbuni
B. fola
C. koto
D. tapisho.

19. **Andika usemi halisi wa sentensi ifuatayo.**
Nokoa alisema kwamba angewaleta vibarua zaidi siku ambayo ingefuata.
A. "Kesho ninawaleta vibarua zaidi," Nokoa alisema.
B. "Tutawaleta vibarua zaidi kesho," Nokoa akasema.
C. "Angewaleta vibarua zaidi kesho," Nokoa alisema.
D. "Kesho nitawaleta vibarua zaidi," Nokoa alisema.

20. Kipi ni kivumishi kilichoundwa kutokana na nomino?
A. Uboreshaji - bora
B. Mwajiri - ajira
C. Mpishi - pikia
D. Refusha - urefu

21. Neno '**walituhesabia**' lina silabi ngapi?
A. 7
B. 6
C. 13
D. 12

22. Chagua sentensi inayoonyesha hali timilifu.
A. Wageni wangefika mapema tungeanza sherehe.
B. Usipojiingiza katika maovu hutapatwa na madhara.
C. Mvua ya masika haijanyesha mapema mwaka huu.
D. Viti vilivyoletwa havitakaliwa na watoto.

23. **Upi ni udogo wa sentensi ifuatayo?**
Gari hilo ndilo lililowabeba wanawali hawa.
A. Kigari hicho ndicho kilichokibeba kijanajali hiki.
B. Vigari hivyo ndivyo vilivyovibeba vijanajali hivyo.
C. Vigari hivyo ndivyo vilivyobeba janajali hilo.
D. Kigari hicho ndicho kilichovibeba vijanajali hivi.

24. Ni maelezo yapi yaliyo sahihi?
A. Faa ni kuwa na maana lakini vaa ni kibao cha kufungia kamba ya tanga.
B. Chaa ni kikundi cha walimaji lakini jaa ni kufika mahali fulani.
C. Shinda ni kuwa wa kwanza lakini shida ni kitu ambacho hakijajaa.
D. Zusha ni kuanzisha jambo lakini chusha ni aina ya mkuki wa kuvulia samaki.

25. Nahau '**pasuka moyo**' ina maana ya
A. kuaga dunia
B. kushtuka sana
C. kuhuzunika
D. kujuta.

26. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
Niliuona mkufu lakini sikuweza kuunyanyua.
A. Barabara
B. Moshi
C. Siafu
D. Nanga.

27. Bainisha sentensi iliyotumia kiambishi '**ni**' cha kuamuru.
A. Viwekeni vyandarua hivyo pale.
B. Yarabi! Gari limetumbukia mtoni.
C. Maji haya ni moto sana.
D. Musa ameenda akalime shambani.

28. Shairi lenye mishororo miwili katika kila ubeti ni
A. Mloto
B. Tarbia
C. Tathnia
D. Utao.

29. **Kanusha sentensi ifuatayo.**
Shama alitumwa kwao akawaite wazazi.
A. Shama hakutumwa kwao wala hakuwaita wazazi.
B. Shama hajatumwa kwao akawaite wazazi.
C. Shama hatumwi kwao wala kuwaita wazazi.
D. Shama hakutumwa kwao akawaite wazazi.

30. **Chagua methali yenye maana sawa na hii.**
Teke la kuku halimwumizi mwanawe.
A. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi.
B. Zimwi likujualo halikuli likakumaliza.
C. Ukupigao ndio ukufunzao.
D. Mwana humwua mzee, mzee hamwui mwana.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Ukiwauliza vijana wengi wa siku hizi, huenda wakakuambia kinagaubaga kuwa hakuna jambo linalowachukiza maishani kuliko kudhibitiwa na wazazi. Watakutolea orodha ndefu ya sheria kali wanazolazimika kufuata kuanzia nyumbani, shuleni, mahali pa ibada na kwingineko. Jambo hili ni kero kwa vijana hivi kwamba wapo wanaoingilia matumizi ya dawa za kulevya almradi wapate <u>kujirutukusha</u> kutokana na <u>kile wanachokiita dhuluma za wazazi</u>. Jambo la kusikitisha ni kuwa wengine, kwa kutowahiwa kwa nasaha ifaayo, huweza hata kufikia uamuzi wa kujitia kitanzi.

Jambo wasilolitambua na kuwazia vijana hawa ni kuwa maisha yamejaa sheria ambazo tunazifuata kila uchao hata pasipo kujua. Hebu fikiria kwa mfano, kuna mtu anayekulazimisha kula, kuoga au kuenda haja? Bila shaka jibu la swali hili unalijua. Kuwazia matokeo ya kukiuka sheria fulani ndiko kunakomfanya mtu kutii bila kuuliza maswali. Hivyo ndivyo zinavyofaa kuwa hata zile sheria za nyumbani au mahali pa kazi.

Kutofuata sheria maishani kuna madhara chungu nzima. Wapo vijulanga ambao, kwa kudai kuwa sheria inawapa haki ya kudhulumiwa, 'hujinyakulia' uhuru au huishia kuwatumbukiza kisimani. Pamoja na hawa ni wale wanaoingilia uraibu wa mihadarati na mapenzi kiholela. Matokeo ya vitendo hivi ni kulia na chanda kili kinywani. *Inasikitisha* kuona tukiwapoteza vijana wachanga kutokana na madhara ya uavyaji mimba, magonjwa ya zinaa na ajali zinazochangiwa na ulevi. Wengi nao wanajutia gerezani baada ya kushiriki vitendo ambavyo viliwapelekea kujipata upande ulio mkabala wa sheria. Lau wangezingatia nyaadhi za wazazi, vijana hawa wangekuwa shuleni au vyuoni wakijiendeleza kimasomo na kitaaluma ili waifae jamii baadaye.

Upo ushauri wa aina nyingi na kanuni ambazo ni muhimu katika maisha ya kila siku. Hata hivyo kwa baadhi ya watu, kuzikiuka sheria hizi huwa ada. Ni mara ngapi tumeshauriwa kuhusu umuhimu wa lishe bora lakini tukajitia hamnazo? Chambilecho wahenga, majuto ni mjukuu baadaye huja kinyume. Si ajabu kwamba hospitali zetu zimefurika furifuri waja wanaotafuta huduma kutokana na kuathirika kisiha. Hii ni licha ya elimu kutolewa kote kuwa njia kuu ya kutunza rai zetu ni lishe bora na kuandama hulka zifaazo. Matokeo ya jambo hili ni kuwa rasilimali nyingi hutumika kugharimia matibabu na kukwamisha juhudi zetu za kujiendeleza.

<u>Ukiona vyaelea jua vimeundwa</u>. Hatuwezi kuwa raia waadilifu iwapo hatutatii sheria za nyumbani tangu tukiwa wadogo. Jamii imara inawahitaji adinasi waadilifu wanaojali hisia za wenzao wanaojistahi na walio tayari kuwajibika kama jamii yao inavyowahitaji. Ukaidi hauwezi kujenga jamii thabiti bali huporomosha misingi yote iliyowekwa ya kuzisimamisha jamii zetu.

Wavyele nao wanahimizwa kuepuka utawala wa mabavu. Kusemezana huleta maelewano. Ni muhimu tuwaketishe kitako vijana wetu na kuwaeleza manufaa ya kuandama mienendo mizuri maishani. Kuwasukumia tu sheria pasipo kuwashauri ipasavyo kunaweza kuzaa ukaidi miongoni mwao.

31. Ni kweli kusema kuwa
A. mwandishi amewahoji vijana kuhusu mambo yanayowachukiza
B. wengi wanawachukia wazazi wanaoingilia uhuru wa vijana
C. mienendo ya vijana hudhibitiwa katika maeneo mbalimbali
D. nyumbani ndiko kwenye sheria zinazochukiza zaidi.

32. Mwandishi wa makala anasema kuwa
A. ushauri ukitolewa kwa wakati ufaao unaweza kuzuia kutokea kwa maafa
B. wengi wanaotumia dawa za kulevya ni wale wanaonyimwa uhuru wao
C. nasaha zikitolewa ulevini vijana watasahau kuhusu vitisho vya wazazi
D. tukiwapa vijana uhuru wanaotaka tutaepuka maovu mengi katika jamii.

33. Maneno '**kile wanachoita dhuluma za wazazi**' yanaonyesha kuwa
A. matendo ya wazazi kwa wanao ni ukiukaji wa haki
B. mwandishi hakubaliani kuwa matendo ya wazazi ni dhuluma kwa vijana
C. ni wazi kuwa wazazi wengi ni katili kotekote
D. mwandishi ana imani kuwa vijana wamekataa kudhulumiwa.

34. Wazo kuu katika aya ya pili ni kuwa
A. mtu akijua kuwa amewekewa sheria ni rahisi kukaidi
B. sheria nyingi maishani zinahusu jinsi mtu anavyokula
C. sheria zinazopatikana nyumbani huchunguzwa mahali pa kazi
D. zipo kanuni tunazozingatia kila siku bila kuziwazia.

35. Chagua maelezo yaliyo sahihi kwa mujibu wa kifungu.
A. Mtu akipewa uhuru anaotamani huishia kuwa kero kwa wengine.
B. Wanaopata uhuru maishani husikitikia maisha yao ya kisogoni.
C. Mtu akipata utulivu anaotamani huelewa maana ya kutodhulumiwa.
D. Matendo yetu ya sasa yanaweza kutuletea huzuni baadaye.

36. Watu wanaopuuza ulaji wa lishe bora
A. hujipata mkabala wa sheria na kukimbilia hospitalini
B. hukimbilia hospitalini na kukumbuka ya wahenga
C. hupoteza rasilimali zao na kukosa kupiga hatua
D. huathirika kiafya na kukosa huduma hospitalini.

37. Methali '**Ukiona vyaelea jua vimeundwa**' inaonyesha kuwa
A. wanaotii sheria wakiwa wadogo huinukia kuwa watu wa kutegemewa katika jamii
B. wanaopuuza sheria wakiwa wadogo hukosa kujali hisia zao
C. wananchi waadilifu ni wale waliodhulumiwa wakiwa wadogo
D. wanaojali hisia za wenzao huzingatia watoto walivyolelewa zamani.

38. Manufaa ya elimu kulingana na kifungu hiki ni
A. kupata kazi na kutegemewa na familia
B. kujiendeleza na kusaidia jamii
C. kuepuka mienendo isiyofaa na kujiunga na vyuo
D. kuzingatia maadili na kuzijua sheria.

39. Kifungu hiki kimependekeza yote haya yafanyike ila
A. sheria zitekelezwe kwa njia ya maafikiano
B. tuwazie madhara ya kukiuka sheria ndipo tuone umuhimu wa kuwajibika
C. vijana wakabiliane na wazazi katika kutetea haki zao
D. ushauri utolewe kwa vijana ili wazingatie mienendo ifaayo.

40. Neno '**kujipurukusha**' jinsi lilivyotumika lina maana ya
A. kujisahaulisha
B. kujiepusha
C. kujikumbusha
D. kujiliwaza.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 – 50.***

Baridi shadidi ya alfajiri ilitupata pale pambajioni tukisubiri zamu yetu ya kuonana na mheshimiwa mbunge wetu. Mama **alijishika tama** huku mawazo mchafukoge yakimwenda mbio akilini. Sijui hii ilikuwa safari ya ngapi kuja mahali hapa. Hata hivyo, kila mara tuliambulia kidole gutu huku tukipewa miadi ya kurejea wakati ujao. Pale tulipoketi, walikuwepo waja wengine ambao aidha waliletwa pale na matilaba yao. Sisi tulikuwa pale kujaribu bahati kuhusu udhamini wa masomo yangu.

Zamu yetu ilipofika, mhazili aliichukua fomu yangu akaisoma. Alitufungulia mlango tukaingia katika ofisi iliyopambwa vyema kwa samani za kisasa. Thamani ya vyombo hivi ililandana kama shilingi kwa ya pili na hadhi ya yule tuliyempata pale. Aliyasikiliza maneno ya mama ambaye alimweleza kuwa alikuwa amefika mahali pale mara kadhaa japo ni mara ya kwanza kupata nafasi ya kumwona mheshimiwa. Baada ya kusikiliza kwa makini mwenyeji wetu alitueleza kuwa ombi letu lisingewezekana kwa wakati ule kwani kasma ya kustawisha maeneobunge iliyotolewa na serikali ilikuwa kichele sana. Tulipoondoka pale, nilikuwa nimeenda nguu kabisa. **Sasa nilikuwa na uhakika kuwa dau langu la masomo lingegonga mwamba.**

Tulifika kiamboni tukiwa hoi. Sikuwa hata na hamu ya kula. Juhudi za mama za kunidekudeku na kunikumbusha kuwa 'Ni heri kufa macho kuliko kufa moyo' ziliangukia masikio yaliyotiwa nta. Nilijifungia chumbani na kulia kama mtoto.

Jioni ilipofika, niliusikia mlango wa mbele ukifunguliwa. Mara nikamsikia mama amepiga vigelegele vya shangwe. Hapo nilivamiwa na shauku ya kupeleleza kiini cha furaha hiyo. Nilipofika sebuleni, baba alinikabidhi hundi ya shilingi laki moja. Nilichanganyikiwa niseweze kuelewa alikozipata fulusi nyingi kiasi kile. Ghafla niliingiwa na dhiki kwa kutuhumu kuwa huenda baba alikuwa amelipiga mnada shamba letu. "Je, ndugu zangu wataishi vipi? Tutapata makazi mengine?" Nilijisaili.

Ni katika hali hii ambapo baba alitueleza kinagaubaga kuwa hundi ile ilitokana na mchango wa mwajiri wake na wafanyakazi wenzake. "Ala! Kumbe watu wenye moyo wa wema na utu wangalipo?" Nilishangaa. Hata hivyo, baba alisema kuwa nilihitajika kutembea pale kazini ili nieleze jinsi nitakavyozilipa fulusi zile. Japo nilikuwa na wasiwasi kwa kutokuwa na jibu sahihi la kuwapa nilijikaza kisabuni na kujikumbusha kuwa mbwa hafi maji aonapo ufuko.

Siku iliyofuata nilifika pale tayari kujieleza. Niliwafahamisha kuwa nisingeisahau hisani yao, kwamba ningeinamia cha mvungu ili nifaulu masomoni na kufanikiwa maishani. Kwa njia hiyo ningewafaa wale wenye mahitaji katika jamii yangu. Isitoshe, ningehubiri uadilifu kwa matendo na maneno yangu ili niwe taa ya kuwaangazia walio nyuma yangu kiumri. Labda baadaye ningepata kiasi cha kuwalipa.

Nilipohitimisha maneno yangu, wote walishangilia kwa furaha. Mwajiri yule alinipiga pambaja akasema, "Ama kweli tunda halianguki mbali kutoka kwenye mti. Naona Bwana Adili amekulea vyema. Bila shaka ukitimiza yale uliyotuahidi utakuwa umetulipa hata pasipo kutoa fedha zozote". Baadaye nilipewa zawadi kochokocho kisha baba akanirudisha nyumbani kufanya maandalizi ya kuenda shuleni. Moyoni nilijua kwamba safari iliyokuwa mbele yangu ilihitaji uwajibikaji mkubwa.

41. Kulingana na aya ya kwanza
A. pambajioni palikuwa na baridi kuliko sehemu zingine
B. huenda kuna watu waliomtangulia msimulizi na mamaye
C. hamu ya kumwona mheshimiwa ilimtia mama mawazo tele
D. msimulizi alijua kuwa safari yao haingeleta manufaa yoyote.

42. Inaonekana wazi kuwa
A. watu waliofika pale walitaka udhamini wa kimasomo
B. wengi waliofika pale waliandamana na wazazi wao
C. mheshimiwa anajua kuwa si mara ya kwanza kwa mama kuomba msaada pale
D. msimulizi na mama yake walikuwa wamefika pale awali ila hawakusaidika.

43. Si kweli kusema kwamba
A. samani zilifanana na kile alichovaa mheshimiwa
B. ofisi ya mheshimiwa ilikuwa imepambwa vizuri
C. hadhi ya mheshimiwa iliambatana na wadhifa wake
D. msimulizi na mama yake hawakufungua mlango wa ofisini.

44. Msimulizi ameeleza wazi kuwa
A. serikali haikuwajibika kwa kukosa kutoa pesa za maeneobunge
B. kama awali, juhudi zao ziliambulia patupu
C. ubaguzi ndio uliomfanya asisaidike ofisini
D. kutosikilizwa ofisini kulimfanya mama ahuzunike.

45. '<u>Sasa nilikuwa na uhakika kuwa dau langu la masomo lingegonga mwamba.</u>' Kauli hii inaonyesha kuwa msimulizi
A. ana msimamo thabiti
B. ni mwenye uhakika
C. ni mwenye kukata tamaa
D. hamwamini mtu yeyote.

46. Mama wa msimulizi ni mlezi mwema kwa sababu
A. anajali hisia za mwanawe na kumtia matumaini
B. anaenda kwa mheshimiwa licha ya kutofanikiwa awali
C. anajua kuwa mtu hafai kukata tamaa kwa lolote
D. anamhimiza msimulizi ale licha ya kuwa hana njaa.

47. Msimulizi hakuonyesha furaha awali licha ya pesa kupatikana kwa kuwa
A. alikumbuka jinsi walivyodhalilishwa na mheshimiwa
B. tayari alikuwa amechelewa kuingia katika shule
C. baba alimfahamisha kuwa angelipa yeye mwenyewe
D. alidhani zilipatikana kwa hali ambayo ingeiletea familia dhiki.

48. Ipi si kati ya ahadi alizoweka msimulizi?
A. Kuwasaidia walio na mahitaji katika jamii.
B. Kujitahidi masomoni ili apate ufanisi.
C. Kuwalipa pesa pindi tu atakapohitimu masomo.
D. Kuwa kielelezo kwa vijana katika jamii.

49. Aya ya mwisho inaonyesha kuwa
A. baba alionyesha uwajibikaji mzuri pale kazini
B. wenzake baba wanazijua tabia njema za msimulizi
C. baba alijua kutoka awali kuwa mwanawe angesaidika
D. mwajiri wa baba alihitaji hakikisho kuwa angelipwa.

50. Msemo '<u>Kujishika tama</u>' kama ulivyotumika katika kifungu una maana ya
A. kuwa na hofu nyingi
B. kuwa na matumaini makubwa
C. kukata tamaa kabisa
D. kuwa na mawazo mengi.

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako**

***Malizia insha yako kwa maneno haya:***

...............................................*ndiposa tukasema kwamba ufisadi lazima ukomeshwe.*